

MPITO: MWANZO MZURI WA SHULE

Miongozo ya kusaidia familia
kukamilisha Taarifa ya Mafunzo ya
Mpito na Maendeleo

KWA NINI MWANZO MZURI WA SHULE NI MUHIMU?

Mwanzo mzuri wa shule husababisha matokeo bora ya mafunzo na ustawi kwa mtoto wako. Unaweza:

- kuepuka usumbufu kwa masomo na maendeleo yao
- kusaidia mtoto wako kujisikia salama, kujiamini na kushikamana.
- kukuza ustahimilivu.

NINI MAANA YA TAARIFA YA MAFUNZO YA MPITO NA MAENDELEO

Taarifa ya Mafunzo ya Mpito na Maendeleo (inayojulikana kama Taarifa ya Mpito) imeandikwa kwa kila mtoto anapohama kutoka huduma ya chekechea hadi shuleni. Taarifa ya Mpito inafanya iwe rahisi kushiriki taarifa kati ya huduma, shule na familia.

Taarifa ya Mpito ya mtoto wako itajumuisha:

- jina la mtoto wako, tarehe ya kuzaliwa na picha
- jina lako na maelezo ya mawasiliano
- jina na maelezo ya mawasiliano ya huduma ya chekechea na wataalamu wengine wa mapema wa utotoni ambao wanasaidia mtoto wako
- habari kuhusu maslahi ya mtoto wako, ujuzi na uwezo
- mikakati ya kufundisha ili kusaidia kujifunza kwa mtoto wako.

Taarifa hizi husaidia mtoto wako na mwalimu wa maandalizi kupata kujua mtoto wako na kupanga masomo yake. Taarifa ya Mpito inaweza pia kukusaidia kuelewa, kusaidia na kujadili masomo ya mtoto wako anapozana shule.

Ikiwa mtoto wako atakwenda kwenye Utunzaji wa Nje ya Saa za Shule (OSHC), Huduma ya OSHC pia itapewa nakala ya Taarifa ya Mpito.

Taarifa ya Mpito ya mtoto wako husaidia:

- kupanga maslahi ya mtoto wako
- kusaidia mabadiliko mwanana kutoka kwa huduma chekechea ya mtoto wako hadi shuleni.

MAWAZO YAKO KATIKA TAARIFA YA MPITO

Unaweza kumsaidia mtoto wako kuwa na mwanzo mzuri wa shule kwa kuchangia taarifa yake ya Mpito.

Taarifa za Mpito ina sehemu za watu tofauti kuweza kujaza.

Sehemu ya 1 na 1.1 zinakamilishwa na mwalimu wa chekechea wa mtoto wako.

Sehemu 1.2 inaweza kukamilishwa na mwalimu wa chekechea wa mtoto wako ikiwa mtoto wako ana ucheleweshaji wa ukuaji au ulemavu. Wataalamu wengine wa utotoni ambao wanasaidia mtoto wako pia wanaweza kuchangia.

Sehemu ya 2: Mtoto inakamilishwa na mtoto wako, akisaidiwa na mtu mzima anayefahamika kama wewe au mwalimu wa chekechea.

Sehemu ya 3: Familia inapaswa kujazwa na wewe. Inauliza maoni yako muhimu kuhusu:

- maslahi ya mtoto wako
- matumaini yako, matakwa na malengo ya mtoto wako shuleni.

Habari hii inaweza kumsaidia mwalimu wa mtoto wako (na mwalimu wake wa OSHC, ikiwa anaye) kuwasiliana na wewe na mtoto wako na kusaidia mafunzo na maendeleo ya mtoto wako.

KITU GANI KINAFUATA BAADAYE?

Rudisha Sehemu ya 3 iliyokamilishwa (na Sehemu ya 2, ikiwa ulimsaidia mtoto wako nayo) kwa mwalimu wa chekechea wa mtoto wako.

Wataweka pamoja sehemu zote za Taarifa ya Mpito na kutoa nakala kwa:

- wewe
- shule ya mtoto wako
- huduma ya OSHC ya mtoto wako, ikiwa anayo.

Kama hujachagua shule bado, utapewa nakala ya pili ya Taarifa ya Mpito. Unaweza kutoa nakala hii kwa shule unapomwandikisha mtoto wako.

Ikiwa hutarudisha Sehemu ya 3, mwalimu wa chekechea bado atashiriki taarifa iliyobaki ya Mpito iliyokamilika na

wewe, shule ya mtoto wako na huduma ya OSHC ya mtoto wako, ikiwa anayo.

Kushiriki maelezo katika Taarifa ya Mpito husaidia watoto mpito kufanikiwa shuleni. Hata hivyo, ikiwa hutaki Taarifa ya Mpito kushirikiwa na shule ya mtoto wako, tafadhali ongea na mwalimu wa chekechea wa mtoto wako.

Wakati mwingine elimu ya Victoria na wataalamu wa utunzaji wanahitaji kushiriki habari ili kulinda ustawi wa mtoto au usalama. Huduma yako ya elimu ya chekechea inaweza kushiriki habari kuhusu mtoto wako na familia pale inapohitajika ili kutimiza wajibu wake wa utunzaji, kupambana na ubaguzi, afya na usalama wa kazi, na majukumu ya ustawi wa mtoto na usalama. Kwa habari zaidi tembelea, <https://www.vic.gov.au/information-sharing-schemes-and-the-maram-framework>

KWA HABARI ZAIDI

Tafadhali tembelea

www.education.vic.gov.au/transitiontoschool

Waraka huu unapatikana katika lugha tofauti kwa

www.education.vic.gov.au/transitiontoschool.